



ST. JOSEPH UNIVERSITY

In Tanzania

VICE CHANCELLOR'S OFFICE

P.O.BOX.11007 Plot no 111&113,
Kibamba "B" Dar-Es-Salaam, Tanzania
Phone: +255748 400 379
Email: vc@sjuit.ac.tz

Ref: VC/SJUIT/ACA/1223/152

29 Agosti 2023

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UDAHILI WA WANAFUNZI WA SHAHADA YA UDAKTARI

Chuo Kikuu cha **ST. JOSEPH UNIVERSITY IN TANZANIA** (SJUIT), kimeona katika mitandao ya kijamii, taarifa ya malalamiko kuhusu udahili wa wanafunzi, hususani kuhusu wanafunzi wanaoomba kujiunga na Chuo Chetu cha Afya na Sayansi Shirikishi (SJCHAS). Imeelezwa kwamba baadhi ya vyuo vinaingia kwenye mfumo wa kujiunga na vyuo na '**kuthibitisha**' kwa niaba ya mwanafunzi.

Aidha, mdau mwingine ametoa mfano akidai Chuo Chetu cha SJCHAS kimeweka utaratibu wa kutaka kila mwanafunzi aliyetuma maombi kulipa ada ya Tsh. Million 2 na gharama nyingine Tsh.500,000 ndipo apewe kiunganishi '[link](#)' cha kujiunga kwenye mfumo wetu.

Chuo Kikuu cha SJUIT kinapenda kueleza kwamba hakina utaratibu wa kuingia katika mfumo na kuthibitisha kwa niaba ya mwanafunzi. Mwanafunzi mwenyewe ndiye mwenye ruhusa ya kuthibitisha kujiunga na Chuo kwa kutumia jina lake (*username*) na nywila (*password*) yake mwenyewe.

Aidha, SJCHAS hakikuweka na wala hakina utaratibu wa kutaka kila mwanafunzi aliyetuma maombi kulipa ada au gharama nyingine kabla ya muda wa usajili.

Chuo kikuu cha SJUIT kinapenda kuwataarifu wanafunzi, wadau na wananchi wote kwa ujumla kwamba taarifa zilizoandikwa si za kweli. Endapo itatokea mwanafunzi aliyetuma maombi akatakiwa kulipa fedha zozote kabla ya muda wa usajili, tunaomba atoe taarifa moja kwa moja Ofisi ya Makamu Mkuu wa Chuo kupitia Simu namba: 0689-304186, email: vc@sjuit.ac.tz au info@sjuit.ac.tz.

Mawasiliano yote kuhusu udahili wa wanafunzi yatafanyika kwa kutumia namba zifuatazo: 0784-757010, 0713-757010, 0699-635000, 0746-516836, na email: admission@sjuit.ac.tz.

IMETOLEWA NA OFISI YA MAKAMU MKUU WA CHUO
ST. JOSEPH UNIVERSITY IN TANZANIA
TAREHE 29 AGOSTI 2023.